

**Biblia inasemaje....?**  
**Yesu aliachukuliaje maandiko?**  
**Sehemu ya sita**

“Mjaribu akamjia akamwambia, ukiwa ndiwe mwana wa Mungu, amuru kwamba mawe haya yawe mikate. Naye akajibu akasema, Imeandikwa, mtu hataishi kwa mkate tu ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu” (Matthew 4:3-4).

Tafadhali zingatia kuwa Yesu alitumia ufahamu wake wa maandiko nyakati za majaribu. Mara baada ubatizo (Mathayo 3), Yesu alifunga siku arobaini mchana na usiku nyikani. Kwa kujua kuwa Yesu amedhoofika kimwili, Ibilisi alijaribu kuitumia hiyo hali kama upenyo kwake kwa kuhoji uungu wa Yesu “Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, amuru kwamba mawe haya yawe mikate” Mara Yesu akanukuu Kumbukumbu la Torati 8:3, kwa kumkumbusha Ibilisi kuwa si “mkate tu” ndiyo tunachohitaji.

Yesu alipata nguvu kutokana na maneno ya Musa. Musa aliyasema maneno haya alipokuwa anawafundisha wana wa Israeli kuhusiana na uweza mkuu unaoshikilia uhai. Mana aliywapa ilikuwa kwa ajili ya kuwafundisha unyenyekevu na kumtegemea Mungu na kwamba Mungu ndiye chanzo cha maisha ya kweli. Yesu alitumia maneno haya ya Musa ili kufundisha kuwa hakuna kilicho muhimu kuliko kumtii Mungu. Hata akiwa katika hali ya uchovu na njaa, Yesu asingeweza kuutimizia mwili mahitaji kabla ya kuyatimiza mahitaji ya roho.

Kwa maneno yake na vitendo vyake Yesu anatufundisha jinsi ya kuyaelewa maandiko na jinsi ya kuyatumia maneno ya Mungu katika kuweka vipaumbele vya matukio maishani mwetu. Kwa kunukuu Kumbukumbu 8:3, sio tu aliihibitisha mamlaka ya Biblia, pia alithibisha kuwa neno la Mungu lilikuja ili kututawala na kutupeleka kwa Baba! Kanisa la Kristo linaamini katika mamlaka ya Neno Takatifu na linatafuta kwenye Biblia majibu ya maswali ya changamoto za maisha.

Sasa, unalipokea neno la Mungu kama mamlaka kwa maisha yako ya kila siku? Unatambua kuwa Yesu anatufundisha waziwazi kuwa daima tunatakiwa kuyatanguliza mahitaji ya kiroho kuliko mahitaji ya mwili?